

MTANZANIA JUMAMOSI JANUARI 21, 2012

Ujerumani yaamua kuipiga jeki CHADEMA

Na Elizabeth Hombo

Dar es Salaam

SERIKALI ya Ujerumani, itakisaidia Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) fedha za kuandaa sera endelevu ya utunzaji wa mazingira na kuondokana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina ya namna ya kuweka sera ya utunzaji wa mazingira nchini, Mwakilishi wa Serikali ya Ujerumani, Stefan Reith, alisema Chadema itapewa msaada wa fedha ili kudumisha ushirikiano wao kupitia semina, mikutano, mafunzo na kutoa ushauri. Hata hivyo kiasi halisi cha fedha hakukitaja.

Pamoja na kutolewa msaada huo, alisema CCM nao wanapata msaada kutoka moja ya shirika la kijerumani kwa muda mrefu.

Katibu Mkuu wa Chadema, Dk Wilbrod Slaa, alisema watu wasiokitakia mema chama chao pindi wanapopata ufadhili kutoka kwa wahisani wamekuwa wakisema kuwa wanaitumia kufanyia maandamano.

"Sisi tunafadhiliwa na Wajerumani ili kuleta maendeleo ya Watanzania, lakini watu wasiotutakia mema wamekuwa wakizungumza kinyume kwamba tunapata msaada hiyo ili kufanyia maandamano. "Misaada kama hii inapopitia kwa Serikali inakuwa ni sawa lakini ikipitia kwa Chadema inakuwa ni nongwa. "Ninawaomba Watanzania wasipumbazwe na propaganda

ambazo hazina tija. Sasa tutaweka pamba kwenye masikio yetu kuzuia propaganda hizo za kututakia ubaya, watafanya hivyo, lakini sisi tutasonga mbele kuwasaidia wananchi," alisema Dk Slaa.

Alisema serikali inapopata msaada kutoka kwa wahisani hawazungumzi, lakini Chadema wanapofadhiliwa wanadai wanafanyia maandamano na vurugu jambo ambalo si la kweli.

Alisema alisema lengo la kuandaa semina hiyo ni kujadiliana na wadau na wataalam wa mazingira kuhusu namna ya kufanya ili kuondokana na mabadiliko ya tabianchi. "Lengo la semina hii tunaandaa sera endelevu ya utunzaji wa mazingira, tutaendelea kufanya semina kama hizi sehemu mbalimbali, tutajadiliana hadi hapo tu-

takapopeleka Kamati Kuu na kujadiliana ili ipatikane sera hiyo ambayo ndiyo itakuwa ilani yetu ya kuhifadhi mazingira," alisema.

Alisema Serikali itekeleze majukumu yake na ipunguze mikutano ya kimataifa ambayo haina tija kwa wananchi.

Hata hivyo, alisema maisha bora hayaletwi na hotuba za jukwaani bali namna ya kuweka mikakati ya namna ya wananchi kupata chakula, maji na umeme.

"Maisha bora yanaletwa na uwajibikaji wa serikali, kuweka mikakati mbalimbali ya kuhifadhi mazingira.

"Tumejaliwa kuwa na ardhi nzuri, maziwa, mito lakini hilo hawalizungumzii bali kuwatanzania tu wananchi kuhusu maisha bora, yako wapi sasa?, kupitia ufadhili huu, Chadema tutaanza uwajibikaji

wa kutunza mazingira," alisema Dk. Slaa.

Kuhusu atakayechukua nafasi ya Mbunge wa Viti Maalum, Regia Mtema aliyefariki wiki iliyopita kwa ajali ya gari, Dk Slaa alisema hilo ni jukumu la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo itaangalia kwenye orodha ya majina ya wabunge yaliyowasilishwa na chama hicho Septemba 30, 2010.

Alisema Chadema ilitumia taratibu za kisayansi ambapo waliwasilisha majina 102 ya wabunge kwa tume hiyo.

"Kati ya majina hayo 102 tuliyowasilisha, wabunge 25 ndio walichaguliwa, hivyo tume itaangalia anayefuatia, yaani wa 26 kama ana sifa ya kuchukua nafasi hiyo na baadaye watatuandikia barua kujua kama huyo wa 26 bado ni mwanachama wetu au la," alisema Dk Slaa.